17:1-21:25 MACHAFUKO KATIKA ISRAELI

Hapa mwandishi alimaliza maelezo yake kuhusu utawala wa Waamuzi wa Israeli. Baada ya hay a anaongeza habari za mambo makubwa mawili ambayo, si lazima kuwa yalifululiza kwa mtiririko wa historia katika kitabu chake, lakini yanaonyesha machafuko yaliyokuwepo katika Israeli wakati ule. Haikuwepo serikali kuu ya taifa lote, na warn wa makabila mbalimbali walifanya walivyoona vema wao wenyewe (17:6; 18:1; 19:1; 21:25). Habari zilizoandikwa hapa zinahusu mabadiliko makubwa na ya maana yaliyotokea katika makabila mawili, yaani Wadani na Wabenyamini.

Uhamiaji wa Wadani (17:1-18:31)

Mika aliyeishi katika eneo la Efraimu, alikuwa ameiba fedha za mama yake. Aliposikia habari ya laana kali ambayo mama yake aliweka juu ya mwizi, alifikiri ni bora kukiri kosa lake na kurudisha fedha zile. Hi kuonyesha shukrani yake, mama yake alifanya sanamu ya fedha na kuiongeza katika sanamu nyingine zilizokuwepo katika nyumba yao ya miungu. Kwa kuzidisha ubaya huo, Mika alimchukua mwanawe, Mwefraimu, akamfanya kuwa kuhani wake (17:1-6). Lakini Mlawi mmoja aliyeishi katika eneo la Yuda alipopitia njia hiyo baadaye, Mika alimwajiri awe kuhani badala ya mwanawe (7-13).

Watu wa kabila la Dani hawakuweza kumiliki urithi wa nchi yao karibu na pwani ya Wafilisti wakati wo wote. Walibanwa katikati ya makabila makubwa mawili ya Israeli, yaani Wayuda na Waefraimu, pia walilazimishwa kurudi nyuma kutoka sehemu za pwani kutokana na nguvu za Wafilisti na Waamori. Hivyo Wadani walibakiwa na eneo dogo sana kwa watu wa kabila lao (taz.l:34). Kwa hiyo walituma wajumbe ili watafute eneo bora zaidi ambalo lingefaa kuwa makazi mapya ya Wadani. Katika safari yao wajumbe wale walipita katika eneo la Efraimu, na usiku mmoja walilala kwa Mika (18:1-2). Walimwomba Mika ushauri kuhusu ujumbe wao wakatiwa moyo kwa jibu lake lenye busara (3-6).

Wapelelezi wa Dani walipoendelea na safari yao, walifika Laisha, mji wa kaskazini kabisa mwa Palestina. Huko waliona eneo la kuwafaa, lenye rutuba na maji ya kutosha. Katika eneo hilo watu watulivu waliishi wasiojiandaa kwa mambo ya vita, nao waliishi mbali sana na miji ya pwani, hata kuitia msaada wa watu kama wangeshambuliwa haingewezekana. Wapelelezi wakarudi kwa furaha na kuwaeleza watu wao mambo waliyoyaona. Hivyo baada ya muda mfupi, Wadani walishika njia ya kusafiri kwenda katika eneo lao jipya (7-10).

Njiani walitua tena katika nyumba ya Mika (11-13). Bila kujali wema wake wa awali, walivunja nyumba ya miungu yake, wakaiba sanamu zote, wakamhonga kuhani ili afuatane nao (14-21) Mika alipojaribu kuwazuia, walimtisha kwamba wangemwua kama angejaribu kuwapinga (22-26). Hivyo waliendelea na safari yao mpaka Laisha walipoua watu wote bila huruma na kuteketeza mji wao kwa moto. Kisha wakajenga mji mpya kabisa kadiri ya ramani yao wakauita Dani, wakimtumia kuhani wa Mika na sanamu zake ili kuanzisha dini yao wenyewe ya ibada ya sanamu (27-31).

Vita vya Wabenyamini (19:1-21:25)

Mlawi mmoja ambaye suria wake (yaani mke wake mdogo) alimtoroka, alifika katika eneo la Yuda ili kumtafuta. Baada ya kumkuta na kupatana naye tena, baba yake mwanamke alifurahi sana, hata akajaribu kuwazuia wasiondoke upesi. Hivyo walikaa kwa muda mpaka waliposhika njia ya kurudi nyumbani kwa Mlawi katika eneo la Efraimu (19:1-9).

Katika safari yao ya kurudi walipita katika nchi ya Benyamini. Jioni yake walipotafuta mahaJi pa kulala, waliona vema wasilale Yerusalemu ambapo wenyeji wake walikuwa Wakanaani, bali waendelee mpaka Gibea ambapo wangekuwa miongoni mwa Waisraeli wenzao (10-14). Lakini watu wa Gibea hawakuwa wakarimu, na Mlawi pamoja na suria wake walifikiri kwamba wangepaswa kulala katika uwanja wa mji. Lakini mzee mmoja (Mwefraimu), aliwaona na kuwakaribisha nyumbani kwake (15-21).

Mlawi alipoufurahia ukarimu wa mzee, nyumba ile ilishambuliwa na kikundi cha wanaume wa Kibenyamini wakimtaka mzee amtoe mgeni wake, ili watulize tamaa yao ya ulawiti. Mzee akakataa, lakini badala yake Mlawi aliwapa suria wake. Watu wale wakambaka mwanamke yule kwa nguvu usiku kucha, na asubuhi yake alionekana mlangoni hali amekufa (22-26). Kisha mume wake akakata maiti yake vipande 12 na kuvipeleka katika kila kabila la Israeli. Tendo hilo lilikuwa desturi ya kale ya kuwaita watu wote ili waunganike dhidi ya adui mkali, ambaye katika tukio hilo walikuwa watu waovu wa Gibea (27-30). (Kwa habari inayofanana taz.lSam 1:1-11).

Askari wa kutoka Israeli yote wakakutana ili kuishambulia Gibea (20:1-11). Licha ya watawala wa Gibea kukosa kujaribu kuwaadhibu majambazi, viongozi wa Benyamini waliwatetea. Wabenyamini wote wakaamua kupiga vita dhidi ya makabila mengine 11 (12-17).

Hapo mwanzo vita vilikwenda vizuri kwa Wabenyamini. Wao walijua nchi yao vizuri zaidi kuliko Waisraeli wengine, na katika milima ile idadi kubwa ya Waisraeli hawakuweza kusaidia sana. Zaidi ya hayo, Wabenyamini walipiga vita kwa ajili ya watu wao na eneo lao, ambapo Waisraeli wengine hawakuwa na malengo yo yote ya binafsi. Pia inawezekana kwamba Waisraeli walitegemea idadi yao kubwa (18-25). Haikuwa mpaka Waisraeli walipomlilia Mungu na kukiri kwamba wangehitaji msaada wake, ndipo alipowaahidia ushindi (26-28).

Hata hivyo Waisraeli walipaswa kupanga mashambulio yao vizuri na kuyatekeleza kwa uangalifu ili waweze kufaulu (29-36a). Kisha habari ya vita inaelezwa kirefu zaidi, ili kuonyesha jinsi Waisraeli walivyotekeleza mkakati wao. Jeshi lao kubwa liliwavuta Wabenyamini nje ya Gibea, na baadaye jeshi lingine dogo lilitoka mafichoni na kushambulia mji wa Gibea usioweza kujitetea. Askari wa Wabenyamini waliokamatwa katikati ya majeshi mawili ya Waisraeli waliangamizwa (36b-46). Askari 600 tu wa Benyamini waliweza kutoroka. Wakati huo Waisraeli walisambaza vita vyao katika eneo lote la Benyamini, wakiteketeza miji yao kwa moto na kuua watu (47-48).

Baadaye Waisraeli walisikitika kwa sababu walizidisha hasira yao na kutia hasara kubwa katika harakati yao. Karibu kabila lote la Benyamini lilikuwa limefutiliwa mbali. Wakati huo Waisraeli walitaka kuwajenga Wabenyamini upya. Lakini kwa sababu kabla ya vita Waisraeli walikuwa wameahidiana kwa kiapo kwamba wasingewapa

Wabenyamini binti zao ili waolewe nao, hawakuona njia ya kuwapatia askari wale 600 waliopona wan awake wa kuwaoza (21:1-3).

Kwa hiyo Waisraeli walitafuta njia nyingine ya kuwapatia Wabenyamini wake. Wakashambulia na kuangamiza mji wa Yabesh-giledi, kwa sababu watu wake walikataa kujiunga katika vita dhidi ya Benyamini, wakawachukua wasichana wao. Kwa njia hii walipata wanawali 400 kuwa wake wa Wabenyamini (4-14).

Kisha viongozi wa Israeli walibuni maarifa ya jinsi ya kuwapatia Wabenyamini 200 waliokosa wake zao (15-17). Waliwapa nafasi ya kwenda katika sikukuu ya kitaifa huko Shilo na kuwakamata wasichana bila ya kuomba ruhusa kwa wazazi wao. Ilikubaliwa kwamba kusiwepo na mapigano yo yote, kwa hiyo Wabenyamini hawakuweza kushtakiwa kuwa waliiba wasichana wale, na kwa sababu wazazi hawakutoa ruhusa rasmi kwa wasichana wao kuolewa na Wabenyamini, hawakuweza kulaumiwa kuwa walivunja kiapo chao (18-22). Wanaume walifanya walivyoambiwa wakafaulu (23-24). Ingalikuwa bure kwa wasichana au wazazi wao kutoa mashtaka, kwa sababu haikuwepo serikali kuu ya kuweza kuamua mambo baina ya makabila (25; taz. 17:6; 19:1).